



**JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA**

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU
NA UTAWALA BORA**



Juni 14,2022

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tamko la THBUB kuhusu matukio ya Loliondo

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imepata taarifa kupitia vyanzo mbalimbali vya habari kuhusiana na matukio yanayodaiwa kuendelea katika Tarafa ya Loliondo wilayani Ngorongoro yanayoashiria uvunjifu wa amani na utulivu. Tume pia inatambua taarifa ya Serikali iliyotolewa Bungeni na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa juu ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali na hali halisi ilivyo.

Vilevile, THBUB imepata taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mhe. John Mongella kuhusiana na hali iliyojitokeza wakati wa zoezi la uwekaji wa alama za mipaka ya Pori Tengefu la Loliondo. Taarifa hiyo ilieleza kuwa kundi la watu walidaiwa kuwashambulia kwa mishale Maafisa wa Serikali na Wataalam waliokuwa katika zoezi hilo na kusababisha kifo cha Askari Polisi, Koplo Garlus Mwita Garlus (36) na kumjeruhi askari mwingine. Aidha, kupitia vyombo vya habari Tume imepata taarifa za madai ya baadhi ya watu kujeruhiwa katika tukio hilo.

THBUB inalaani vikali matukio yote yanayoashiria uvunjifu wa amani na utulivu ikiwemo mauaji ya askari na kusababisha majeraha, ambayo ni kinyume na haki za binadamu, pamoja na kauli mbalimbali zinazotolewa na baadhi ya watu.

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere – Kilimani, S.L.P 1049, DODOMA/ Kitalu Na. 201, Mweni, S.L.P 285, ZANZIBAR

Simu: +255 734 047 775/734 119 978 (Makao Makuu); +255 (24) 2230494 (Zanzibar)

Barua Pepe: info@chragg.go.tz, zanzibar@chragg.go.tz; Tovuti: www.chragg.go.tz

Wakati THBUB ikiendelea kulifuatilia suala hili, kwa muda huu inapendekeza yafuatayo:

- i) Serikali iendelee kujadiliana na wananchi na wadau mbalimbali ili kulipatia ufumbuzi suala hilo kwa njia ya amani;
- ii) Serikali iendelee kutoa taarifa kwa umma kuhusiana na hali inayoendelea Wilayani Ngorongoro;
- iii) Jeshi la Polisi lifanye uchunguzi wa matukio ya uvunjifu wa sheria ili kuwabaini wahusika na kuwafikisha katika vyombo vya sheria;
- iv) Wananchi wawe wavumilivu, waheshimu sheria na kutoa ushirikiano kwa watendaji wa Serikali na vyombo vya ulinzi na usalama.

THBUB inaadhi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali, wananchi na wadau mbalimbali katika kulinda, kuhifadhi na kukuza haki za binadamu na utawala bora.

Imetolewa na:



Mohamed Khamis Hamad
Makamu Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Juni 14, 2022